

NINATUBU

Jofrey P. Otayo
Oct. 2024

1. Na ku u nga mi a Mu ngu wa ngu ni me ko sa ni
Na nyi ndu gu za ngu ni na tu bu Mu ngu wa ngu ni

7

me ko sa sa na mi mi kwa ma ne no ma wa zo na - ma te ndo
na tu bu ni sa me he ndu gu za ngu ni na tu bu mni sa me he

2. Na ulimi ulinipa Mungu / nitangazie habari njema / ona kumbe ninanenea uongo / hakika mimi nimekosa-natubu / nifanye kuwa muhubiri wa neno / nitangaze habari njema kwa wote.
3. Nguvu nydingi ulinipa Mungu / nimetumia kutesa watu / nisijue nimepewa kwa malengo / ili kwalo sifa zirudi-kwa Mungu / niwe kama Daudi kwake Go-lia-ti / nikomboe watu wako wateswao
4. Mali pia umenipa mimi / majivuno najikweza mimi / najiona kwamba mimi ndiyeye Mungu / kila kitu Duniani-ninaweza / ninataka niabudiwe na mimi / nimekosa natubu unisamehe
5. Usihesabumakosa yangu / mwili wangu unanuka dhambi / ni-m-chafu nitakase unioshe / nifanye upya niwe-kama kichanga / roho wako a-ni-o-ongoze kutenda / nitende kadiri ya mapenzi yako.
6. Uso wa niukwepe vipi? / adhabu yako ni kwepe vipi? ikiwa mbinguni huko wewe upo / Duniani kote Mungu - wewe upo / ningefanya kuzimu kitanda changu / kote huko wewe unapatikana
7. Roho yangu inakupenda Mungu / mwili wangu ni dhaifu sana / mwili wangu unazidiwa tama-a / kama sumaku nimevutwa na Dunia / mwili wangu hauna kinga ya dhambi / nisaidie nije kwako mbinguni.
8. Ninajikabidhi mbele yako, unilinde maishani mwangu / nifyange unavotaka ee Mungu / nipe yote ninayopaswa kupewa / nisamehe unisamehe dhambi zangu / nimekosa Mungu wangu nimekosa.